# THE ELITE JET

**102/3** **KISWAHILI** **Karatasi ya 3**

## (Fasihi)

## PREMOCK

**Machi 2026 – Saa: 2½**

**No ya Usajili.............................................................. No. ya mtihani.............................**

**Shule .............................................................Tarehe………..Sahihi y...........................**

---

**Maagizo**

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike jina la shule katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali manne pekee.
(d) Swali la kwanza ni lazima.
(e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani, Riwaya, Hadithi Fupi, Ushairi. Na fasihi simulizi
(f) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
**(g) Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.**
**(h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**
(i) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya **Kiswahili.**

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**1 SWALI LA LAZIMA**

## SEHEMU YA A: USHAIRI

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo!Hutaki,
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli miania, kwako ona haitoki,
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Machungu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiliki,
Na tena ukajiona, kuwa wewe mstahiki,
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,
Uliyataka mwenyewe!

**Maswali**

(a) Eleza ujumbe katika shairi hili. (alama 3)
(b) Ukizingatia kigezo kifuatacho, taja aina za bahari za shairi. (alama 2)
(i)Vina
(ii)Kibwagizo
(c) Tambua kwa kutoa mifano mitatu ya mbinu ambazo mshairi ametumia ili kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
(d) Eleza muundo wa ubeti wa tano. (alama 4)
(e) Fafanua umuhimu wa aina mbili za urudiaji. (alama 2)
(f) Bainisha toni ya shairi hili. (alama 2)
(g) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 4)

## SEHEMU YA B: TAMTHILIA

**T.M Arege.:** *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 2 au la 3*

2 ***Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:***

'Alitafunwa kama chingamu lakini naye hakuwa chingamu ya kuisha sukari'

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua umuhimu wa mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4)

(c) Eleza umuhimu wa anayerejelewa katika dondoo hili katika kuijenga tamthilia ya 'Bembea ya Maisha' (alama 12)

***AU***

3 **(a) *Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo*.** (alama10)

(Anajisemea) "Bunju ni mmoja wenu. Nyote ni wanangu" Hayo ni maneno ya mama. Wakati huo sikuona. Sasa ninaona. Wanasema mwenye macho haambiwi tazama. Kweli iliyoje! Japo hutokea wakati tukalalamika, ninafikiri Bunju ni zawadi nzuri kwetu. (Anaikaribia hadhira na kuizungumzia) Leo tungekuwa wapi bila Bunju? Maji yangezidi unga. Usingepikika, usingelika. (Kimya) Hebu fikiri! Umepata ajali mbaya. Inakuacha mahututi. Anapita mtu katika gari lake. Kwa imani anaguswa. Anakufanyia mpango wa Flying Doctors: ndege inafika kukupeleka hospitali. Mwenyewe huyo analipia kila kitu. Ninakwambia kila kitu! Mtu huyo atakosaje kuwa zawadi kwako?"

(b) Asasi ya ndoa inakumbwa na changamoto nyingi katika maisha.Thibitisha kwa kurejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama10)

## SEHEMU YA C: RIWAYA

**Clara Momanyi :** *Nguu Za Jadi*

*Jibu swali la 4 au la 5*

4 ***Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:***

"Nikupe ushauri dada. Kaa mbali naye kwani yule ni moto wa kuotea mbali. Ukimfuatafuata, anaweza kukutendea mambo mabaya. Kumbuka una watoto wanaokuhitaji."

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

(b) Bainisha toni inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

(c) Thibitisha kuwa anayerejelewa ni moto wa kuotea mbali. (alama 9)

(d) Fafanua jinsi mbinu ya majazi imetumika katika kujenga kipengele cha wahusika katika riwaya 'Nguu za Jadi." (alama 5)

5 “Kisisi kilimvaa. Sasa alikuwa akihema pumzi za mjusi. Jasho lilimtiririka usoni kama aliyemwagiwa maji. Alijikwaa miguu ovyo. Kiwiliwili chake kikaanza kuyumba kwa hofu na hawafu.”

(a) Bainisha aina za taswira katika dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua umuhimu wa mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
(c) Thibitisha mandhari ambamo dondoo hili limetolewa. (alama 2)
(d) Eleza toni ya dondoo hili. (alama 2)
(e) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili ukirejelea vipengele vifuatavyo : (alama 10)
  (i) Maudhui
  (ii) Wahusika

## SEHEMU YA D:HADITHI FUPI

**D.M. Lutomia na P. Muthama :** *Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au la 7*

**P.N. Mutua: “ Harubu ya Maisha”**

6 ***Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:***

“Hapakuwa na haja ya kuendelea kulala. Ilinibidi nianze kujiandaa kwenda kazini. Nilipokuwa naoga, niliwazia mabadiliko. Mabadiliko ya hali anuwai za maisha yangu. Niliiwazia hali ya ndoa yangu miaka minne iliyopita. Kila kitu kilikuwa raha, isipokuwa baadaye kidogo wakati wa nyondenyonde za mama Mercy alipokuwa akimtarajia mwanetu kuzaliwa. Mshahara wangu ulikuwa mdogo, lakini ni kana kwamba haukuingia akilini wala kumtaabisha yeyote. Kisha alikuja Mercy. Akaja na mambo yake. Mara meno. Mara mafua. Mara katia punje za mahindi puani au sikioni na kulazimisha miadi na daktari. Wakati ukapita. Mpaka juzi alipojiunga na shule ya chekechea. Sasa anahitaji sare ya shule, kalamu, madaftari, karo na mengine!”

(a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)
(b) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 4)
(c) Tambua nafsi ya usimulizi ya dondoo hili. (alama 2)
(d) Jadili umuhimu wa matumizi ya dayalojia katika hadithi ya Harubu ya Maisha (alama 10)

**D.W. Lutomia “Msiba Wa Kujitakia”**

7 **(a)** Miti katika msitu ilizidi kuangamizwa kwa makali ya shoka lakini miti ilizidi kulifurahia shoka kwa kuwa mpini wake ulikuwa umetengenezwa kutoka kwa kipande cha mti. Miti ikafikiri shoka ni mmoja wao!

(i) Kwa kutoa mfano mwafaka, eleza changamoto zinazowakabili wananchi wa Matopeni kwa mujibu wa hadithi hii. (alama 5)
(ii) Eleza mbinu tano wanazotumia viongozi wa Matopeni kuingia mamlakani. (alama 5)

**Y.S. Hamad “Mzimu Wa Kipwerere”**

**(b)** Yaani kile kitendo cha kichaka kile kuitwa mzimu kilikuwa homa ya jiji na shetani tosha

(i) Eleza umuhimu wa nyimbo katika kujenga hadithi ya Mzimu wa Kipwrere. (alama 4)
(ii) Eleza umuhimu wa mandhari ya Mzimu wa Kipwerere katika kuijenga hadithi hii. (alama 6

## 8 SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata***

Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu.Wanyama hawa waliishi baharini. Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba. Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko, matikitimaji na kadhalika. Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza. Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka. Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

**Maswali**

(a) Tambua utanzu huu na kipera chake. (alama 2)

(b) Eleza sifa tano za utanzu wa kipera hiki. (alama 5)

(c) Eleza umuhimu wa fomyula ya kuhitimisha katika aina hii ya ngano. (alama 3)

(d) Wewe ni fanani anayewasilisha kipera hiki kwa hadhira.Taja mambo matatu ambayo utafanya kuhakikisha umefanikiwa katika uwasilishaji wako. (alama 3)

(e) Taja manufaa mawili ya ngano katika jamii. (alama 2)

(f) Kipera hiki kinaendelea kudidimia katika jamii yako.Eleza mbinu tano utakazozitumia kukidumisha katika jamii ya leo. (alama 5)

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................................................................

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO**